

TANGAZO LA SERIKALI NA. 404 la tarehe 24/5/2024

SHERIA YA USAFIRI MAJINI,
(SURA YA 165)

KANUNI

(Zimetengenezwa chini ya vifungu vya 217 na 222)

KANUNI ZA MAREKEBISHO YA KANUNI ZA UANZISHAJI NA UENDESHAJI WA VIFAA
VYA KUONGOZEA MELI ZA MWAKA 2024

Jina

1. Kanuni hizi zitajulikana kama Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Uanzishaji na Uendeshaji wa Vifaa vya Kuongozea Meli za Mwaka 2024 na zitasomwa pamoja na Kanuni za Uanzishaji na Uendeshaji wa Vifaa vya Kuongozea Meli za Mwaka 2023 ambazo hapa zitarejewa kama “Kanuni kuu”.

TS. Na.
497 ya 2023

Marekebisho ya
jumla

2. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta maneno “vifaa vya kuongozea meli” na “kifaa cha kuongozea meli” popote yanapojitokeza katika kanuni na badala yake kuweka maneno “nyenzo za kuongozea meli” na “nyenzo ya kuongozea meli”.

Marekebisho ya
kanuni ya 2

3. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 2(2) kwa kufuta maneno “inayotokana na malipo ya ada ya vifaa vya uongozaji meli”.

Marekebisho ya
kanuni ya 3

4. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 3 kwa kubadili mpangilio wa tafsiri ya misamiati kwa kuzingatia mpangilio wa tafsiri ya misamiati katika Toleo la Kiingereza la Kanuni hizi.

Marekebisho ya
kanuni ya 7

5. Kanuni kuu zinarekebishwa katika kanuni ya 7 kwa kufuta kanuni ndogo ya (1) na badala yake kuweka kanuni ndogo ifuatayo:

“(1) Shirika litakuwa na mamlaka ya usimamizi wa jumla katika nyenzo za

*Kanuni za Marekebisho ya Kanuni za Uanzishaji Na Uendeshaji wa Vifaa Vya
Kuongozea Meli*

Tangazo La Serikali Na. 404 (Linaendelea)

kuongozea meli katika maji ya Tanzania
na maeneo ya karibu.”.

Kufutwa na
kuandikwa
upya kwa
kanuni ya 19

6. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta kanuni
ya 19 na badala yake kuweka kanuni ifuatayo:

“Utatuzi wa
kushughulikia
malalamiko
kuhusu
uwajibikaji wa
malipo

TS. Na.
338 ya 2018

19. Endapo mtu
anapingamizi dhidi ya ada au
gharama zinazohusiana na nyenzo
za kuongozea meli, ambazo
zinapaswa kulipwa na meli chini
ya Kanuni hizi au pingamizi dhidi
ya kiasi cha ada au gharama hizo,
mtu huyo atapaswa kuwasilisha
maombi kwa Shirika kwa ajili ya
utatuzi wa malalamiko kwa
mujibu wa Kanuni za
Kushughulikia Malalamiko za
Mwaka 2018.”

Kufutwa na
kuandikwa
upya kwa
kanuni ya 21

7. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta kanuni
ya 21 na badala yake kuweka kanuni ifuatayo:

“Msamaha

21. Msajili anaweza kutoa
Notisi ya Usafiri Majini kwa meli
zilizopewa msamaha na mtoa
huduma wa nyenzo ya kuongozea
meli, kulipa tozo kwa ujumla au
kwa kiwango kinachoweza
kuainishwa kwenye Notisi hiyo.”.

Kufutwa kwa
kanuni ya 26

8. Kanuni kuu zinarekebishwa kwa kufuta kanuni
ya 26.

Dodoma,
3 Mei, 2024

MAKAME M. MBARAWA
waziri wa Uchukuzi